JINA……………………………………………… SAHIHI……………………………….

SHULE…………………………………………… NAMBARI YAKO……………………

102/1

KISWAHILI

Karatasi ya 1

INSHA

Machi/ Aprili 2015

Muda: Saa 1 ¾

# MITIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA TARAFA YA KABONDO - 2015

***Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.***

**MAAGIZO**

a) Andika insha mbili
b) Insha ya kwanza ni ya lazima. Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.
c) Kila insha isipungue maneno 400
d) Kila insha ina alama 20

***Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa mwanafunzi anapaswa kuhakikisha kwamba karatasi zote ni sahihi na hakuna maswali yanayokosekana.***

1. Kumekuwa na visa vingi vya mauaji hapa nchini, mhariri wa gazeti la Nyota amewatangazia wasomaji katika toleo la Jumapili kutuma makala yao ili kuchangia katika kuandika tahariri itakayohusu chanzo cha mauaji hayo na suluhisho. Andika makala hayo.
2. Pesa za hazina ya ustawi wa maeneo bunge zapaswa kuondolewa chini ya usimamizi wa wabunge.Jadili
3. Mkono usioweza kuukata, ubusu
4. Andika insha itakayoisha kwa:
   …………………..Nilishusha pumzi, nikashukuru Mola nilipojipata hoi bin taabani miongoni mwa wafu.

JINA…………………………………………… SAHIHI……………………………….

SHULE………………………………………… NAMBARI YAKO……………………

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Machi/ Aprili 2015

Muda: Saa 2 ½

# MITIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA TARAFA YA KABONDO - 2015

***Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.***

Maagizo

1. Jibu maswali **manne** pekee
2. Swali la kwanza ni la lazima
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na fasihi simulizi
4. Usijibu maswali mawili kutoka kutoka sehemu moja.
5. Karatasi hii ina kurasa zilizopigwa chapa
6. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

| SWALI | | | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| ALAMA | | | | | |

***Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa mwanafunzi anapaswa kuhakikisha kwamba karatasi zote ni sahihi na hakuna maswali yanayokosekana.***

**FASIHI**

**SEHEMU A : USHAIRI**

1. **Lazima**

   **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Chema hakidumu,kingapendekeza,
Saa ikitimu,kitakuteleza,
Ukawa na hamu,kukingojeleza,
Huwa ni vigumu,kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi,kwamba nakitweza,
Japo mara tumbi,kinshaniliza,
Na japo siombi,kipate niongeza,
Mtu haniambi,pa kujikimbiza.

Chema mara ngapi, kuniondoka,
Mwanangu yu wapi? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatalika?
Ningefanya lipi, kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, ni nitengenee,
Ilahi wahhabu, mara amtwee.

Chema wangu Poni, kipenzi nyanyangu,
Hadi siku hini, yu moyoni mwangu,
Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
Ningamtamani, hatarudi kwangu
(Abdalla Abdilatif, Sauti ya Dhiki)

Maswali

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (Alama 2)

b) Shairi hili lina bahari zipi? Taja bahari mbili na utoe sababu (Alama 4)

c) Eleza umbo la beti mbili za mwisho (Alama 4)

d) Eleza toni ya shairi hili (Alama 2)

e) Dhamira ya malenga ni nini katika shairi hili (Alama 2)

f) Toa mifano miwili ya matumizi ya mbinu ya inkisari katika shairi hili (Alama 4)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yaliyotumiwa katika shairi (Alama 2)

i. Kinshaniliza

ii. Ela

**SEHEMU B: RIWAYA**

**Ken Walibora : Kidagaa Kimemwozea**

Jibu swali la 2 au la 3

**2.** "Wataka mimi nipike? Ehee? Ati miimii nalaza damu? Wewe unaiamsha damu? Bloody bastard……..

a) Eleza mukhtadha wa dondoo hili (Alama 4)

b) Bainisha mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (Alama 4)

c) Kwa kurejelea riwaya, jadili maudhui yanayoendelezwa na mnenaji (Alama 12)

**3.** Jadili ufaafu wa anwani "Kidagaa Kimemwozea" (Alama 20)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**Ken Walibora na S.A Mohamed: Damu Nyeusi na hadithi nyingine.**

**Jibu swali la 4 au la 5**

"Damu Nyeusi" (Ken Walibora)

4. "Je, kule kwenu watu wanavaa nguo au wanatembea rabana?

a) Eleza mukhtadha wa dondoo hili (Alama 4)

b) Bainisha mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili (Alama 2)

c) Eleza masaibu saba yaliyomkumba mrejelewa ughaibuni Kwa mujibu wa hadithi hii. (Alama 14)

"Gilasi ya mwisho makaburini" (Said A. Mohamed)

5 a) Onyesha matumizi matano ya ishara katika hadithi hii (Alama 10)

b) Fafanua matatizo yanayokumbwa asasi ya ndoa kwa mujibu wa hadithi hizi.

i). Mke wangu (Alama 5)

ii) Mwana wa Darubini (Alama 5)

**SEHEMU D: TAMTHILIA**

**T. Arege: Mstahiki Meya**

6. Haki yetu!
   Jasho letu!
   Haki yetu!
   Jasho letu!
   Damu yetu!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama. 4)
b) Jadili mambo **matano** yaliyosababisha kutokea kwa hali hii (Alama 10)
c) Eleza njia **tatu** zilizotumiwa na wahasiriwa katika dondoo hili kukabiliana na kutoridhika kwao katika tamthilia hii (Alama 6)

7. Kwa kurejelea Tamthilia ya Mstahiki Meya, eleza matatizo Yanayokabili mataifa ya bara la Afrika (Alama 20)

**SEHEMU E: FASISHI SIMULIZI**

8. a) Maagizo ni nini? (Alama. 2)
   b) Eleza mambo mawili yanayofanikisha kutendeka kwa maigizo (Alama 4)
   c) Ngomezi ni nini? (Alama 2)
   d) Fafanua sifa **nne** za ngomezi (Alama 4)
   e) i) Taja shughuli zozote **NNE** zinazohusishwa na Miviga (Alama 4)
   ii) Miviga ina hasara gani katika jamii ya leo (Alama 4)